**HOTUBA YA MHE. GEORGE SIMBACHAWENE (MB.) WAZIRI *WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA* UMMA NA UTAWALA BORA WAKATI WA KIKAO KAZI CHA WACHUNGUZI WA SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA KATIKA UKUMBI WA NGORONGORO ARUSHA TAREHE 18 MACHI, 2024**

***Mhe. Jaji (Mst.) Sivangilwa Mwangesi, Kamishna wa Maadili;***

***Wajumbe wa Managementi wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;***

***Wajumbe wa Kikao kazi;***

***Waandishi wa Habari;***

***Mabibi na Mabwana.***

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania… Kazi iendelee.**

***Ndugu Washiriki;***

Ndugu washiriki wa kikao hiki, awali ya yote nimshukuru Mola wetu

Mtukufu, mwingi wa rehema, kwa kutujalia uhai, afya njema na kutuwezesha kukutana hapa katika ukumbi wa Ngorongoro jijini Arusha kwa ajili ya kujadili mustakabali wa utekelezaji wa majukumu yetu.

Pili, ninawapongeza viongozi wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma chini ya uongozi wa Mhe. Sivangilwa mlioshiriki kuandaa Kikao Kazi hiki na kunialika kushiriki nanyi katika mkutano huu muhimu sana kwa maendeleo ya taasisi. Hii ni mara yangu ya kwanza kujumuika nanyi katika kikao kama hiki tangu nilipoteuliwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kusimamia Wizara hii.

***Ndugu Washiriki;***

Kipekee ninawapongeza watumishi wote wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa kutekeleza majukumu yenu ya kusimamia tabia na mwenendo wa Viongozi wa Umma kwa weledi na umakini mkubwa. Mmekuja kushiriki kakao hiki muhimu kwa lengo la kuwasilisha maoni yenu yatakayosaidia kujenga misingi mizuri ya kitaasisi yatakayosaidia kuboresha mbinu za utendaji kazi na utatuzi wa changamoto mnazokabiliana nazo.

***Ndugu Washiriki;***

Nimeelezwa kuwa kikao kazi hiki kina lengo la kuwakutanisha wachunguzi wote ndani ya Taasisi kujadili kwa kina mambo mbalimbali yanayohusu utendaji wa kazi, mafanikio mliofikia kwa mujibu wa matakwa ya Ibara ya 132 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Katiba imeweka misingi ya Maadili ya Viongozi wa Umma ambapo nyinyi ndio mliopewa jukumu la kuhakikisha inafuatwa.

Jukumu hili ni kubwa na zito kwa sababu ni la Kikatiba na linaifanya Taasisi hii kuwa jicho la Serikali katika kufuatilia tabia na mwenendo wa Viongozi wa Umma ili kuhakikisha kuwa Taifa linaongozwa na watu waadilifu, wanaofuata misingi ya maadili na utawala bora.

Misingi hii ya maadili inalenga kuleta usawa, kutoa haki sawa kwa wote na kuthibiti mmomonyoko wa maadili miongoni mwa Viongozi wa Umma ikiwemo mgongano wa maslahi wanapotekeleza majukumu yao. Misingi hii lazima tuilinde na hili ndilo jukumu letu. Misingi hii isipozingatiwa, wananchi wanakosa huduma na malengo ya nchi kutofikiwa.

***Ndugu Washiriki;***

Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali kuunda vyombo vya usimamizi wa maadili ikiwemo Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ili wananchi wake wanufaike na huduma zinazotolewa na kuwa na imani na Serikali yao. Azima hiyo ya Serikali itafikiwa iwapo kila mtumishi wa Umma **atatimiza wajibu wake.**

***Ndugu Washiriki;***

Kwa sababu hiyo, mnalo jukumu la kutoa elimu kwa Viongozi wa Umma na wananchi ili kila mmoja aijue misingi ya maadili mnayoisimamia. Kuchunguza na kufichua vitendo vya ukosefu wa maadili kwa kushirikiana na wananchi. Hata hivyo, ufanisi wa utendaji kazi wenu unahitaji weledi , kujituma, kuweka mipango madhubuti ya utekelezaji, kuwa na mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu pamoja na vikao kazi kama hiki. Haya yote yatasaidia kuleta ufanisi wa kazi yenu ya kichunguzi na kufikia malengo yaliyokusudiwa wakati wa uanzishwaji wa Taasisi.

***Ndugu Washiriki;***

Katika kikao hiki, nimeambiwa kuwa mtakuwa na mada mbalimbali zikiwemo;

1. Utendaji katika Ofisi za Kanda.
2. Viambata vya Makosa ya Maadili.
3. Utaratibu wa zoezi la Uhakiki.
4. Mikakati ya utendaji kazi pamoja na

5. Changamoto na utatuzi wake katika kushughulikia malalamiko na uchunguzi.

Nimefurahishwa na uwepo wa mada hizi ambazo zinalenga kujitathmini utekelezaji wenu wa majukumu, pamoja na utatuzi wa changamoto mnazokabiliana nazo, na bila shaka baada ya kikao mtajiwekea maazimio ya utekelezaji.

Ni matumaini yangu kuwa kikao hiki kitasaidia kutoa mawazo mazuri kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu yenu, kuleta tija na ufanisi wa kazi katika taasisi na Taifa kwa ujumla.

***Ndugu Washiriki;***

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dr. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inatoa kipaumbele na kuzingatia maslahi ya watumishi wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Wizara pia kwa upande wake imekuwa ikishirikiana na Mwajiri kuhakikisha maslahi ya watumishi yanazingatiwa ikiwa ni pamoja na kuwapatia vitendea kazi na stahili zao ili wafanye kazi kwa ufanisi na kuleta tija. Serikali inapotimiza

wajibu wake, watumishi nao wana wajibu wa kutimiza malengo wanayowekewa na mwajiri **kwa sababu hakuna haki bila wajibu.**

***Ndugu washiriki;***

Ili kufikia lengo hilo la Kikatiba, lazima taasisi iwe na malengo ya muda mrefu na mfupi. Sekretarieti ya Maadili kwa kuzingatia majukumu yake ya Kikatiba na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya mwaka 1995, haina budi kujikita katika Dhima yake ya kuhakikisha utamaduni wa Uadilifu kwa Viongozi wote wa Umma kupitia kukuza na kufuatilia tabia za Viongozi wa Umma na kusimamia mgongano wa maslahi ili kujenga imani kwa umma katika kukuza maendeleo ya Taifa.

Katika kutekeleza jukumu hili, lazima mtumie weledi na busara mnaposikiliza malalamiko ya wananchi dhidi ya Viongozi wa Umma na myafanyie kazi kwa uadilifu wa hali ya juu. Sasa hivi wapo baadhi ya Viongozi wa Umma wanaolalamikiwa kujihusisha na vitendo vya mgongano wa maslahi wanapotimiza majukumu yao. Nawaelekeza kutoa

elimu ya maadili kila mnapopata nafasi ili dhana hii ieleweke vizuri kwa Viongozi na wananchi. Kwa kutumia mbinu za uchunguzi mlizonazo, fuatilieni viongozi wanaojihusisha na vitendo vya ukiukwaji wa maadili ikiwemo mgongano wa maslahi ili haki itendeke, na kwa wale watakaobainika sheria ichukue mkondo wake.

***Ndugu washiriki;***

Ilani ya Chama Tawala, Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 ambao ndio mkataba kati ya Serikali na Wananchi, katika aya ya 112 kiliahidi kuendelea kuhakikisha suala la Maadili ya Viongozi wa Umma linatiliwa mkazo na kuimarishwa zaidi ili wananchi waendelee kunufaika na huduma bora kulingana na matarajio yao. Ili kufikia malengo hayo, Chama kiliahidi kuielekeza Serikali (Sekretarieti ya Maadili) kuchukua hatua zifuatazo:-

a) *Kusimamia nidhamu, uadilifu, uwazi, uzalendo wa kitaifa, moyo wa kujitolea na uwajibikaji miongoni mwa Viongozi na watumishi wa umma;*

b) *Kuongeza watumishi wenye sifa stahiki kwenye utoaji huduma na kuhimiza watumishi wa umma kufanya kazi kwa juhudi, maarifa, ubunifu na weledi katika kujenga taifa letu;*

c) *Kudhibiti migongano ya masilahi katika shughuli za Umma kwa kusimamia mifumo iliyopo; na*

d) *Kujenga jamii inayoheshimu na kuthamini utu, haki, maadili na nidhamu.*

***Ndugu washiriki;***

Hili ni jukumu lenu. Hakikisheni Viongozi wa Umma wanaielewa dhana ya uwajibikaji wa pamoja na kuheshimiana.

***Ndugu Washiriki;***

Nafahamu kuwa Taasisi yenu inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo kwa namna moja ama nyingine zinadhoofisha utendaji wenu wa kazi.

Miongoni mwa changamoto hizo ni ufinyu wa bajeti, Ufinyu wa majengo ya Ofisi, Katika Ofisi/Kanda za Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, isipokuwa Kanda ya Kusini ambapo Taasisi ina miliki jengo lake.  Aidha, Jengo la ofisi ya Makao Makuu na Kanda ya Kati, nina matumaini kuwa katika mwaka huu wa fedha litakamilika. Kanda nyingine zimepanga na zinatumia fedha nyingi kwa ajili ya pango.

Changamoto nyingine ni uhaba wa baadhi ya Vitendea Kazi (Magari) na ukosefu wa watumishi wa kutosha kwa mujibu wa ikama yenu.

Changamoto hizo zote Serikali itaendelea kuzitatua kwa kuzingatia vipaumbele kuanzia mwaka ujao wa fedha wa 2024/25.

***Ndugu Washiriki;***

Nihitimishe hotuba yangu kwa kuwashukuru tena kwa kunialika kufungua Kikao Kazi hiki muhimu, kwa ustawi wa Taasisi yetu pia kuushukuru uongozi wa Sekretarieti ya Maadili chini ya Mhe. Jaji (Mst.) Mwangesi kwa kuwezesha kikao hiki.

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania… Kazi iendelee.**

***ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA***